# Cre8 in 8



cre8 east africa
education through culture & art

**MKAKATI WA HATUA NANE WA KUVISAIDIA VIKUNDI VYA VIJANA KUFIKIA (KUTIMIZA) UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SANAA ZA KIJAMII KWA NJIA JUMUISHI NA SHIRIKISHI**

**Waandaaji**

Mkakati wa Cr8 in 8 uliandaliwa na Sami Gathii, Janneke Tigchelaar na Ben Hekkema

**Maandishi** Sami Gathii, Janneke Tigchelaar, Ben Hekkema, *www.cre8eastafrica.org*
**Ubunifu** Gerrit Alink, *www. gerritalink.nl*
**Uhariri** Thom Johnston, *www. johnston.nl*
**Vielelezo na Michoro** the Hard Life Artists, *Facebook: Hard Life Artists Group*
**Mfasiri** Charles Godfrey Massawe, *camilaca222@gmail.com*
**Picha** Cre8 East Africa (Cre8 Afrika Mashariki)

© Toleo hili linaweza kuchapishwa na kusambazwa. Tafadhali wahusishe Cre8 Afrika Mashariki kama ukifanya hivyo.

# YALIYOMO

**UTANGULIZI** 4

**KUTAMBULISHA MKAKATI WA "CRE8 IN 8"** 6

- **Hatua ya kwanza: MAANDALIZI NA UANZILISHAJI** 8
- **Hatua ya pili: UHAMASISHAJI WA WASHIRIKI** 16
- **Hatua ya tatu: KUJENGA KUNDI** 24
- **Hatua ya nne: UCHUNGUZI WA KISANAA NA UGUNDUZI** 30
- **Hatua ya tano: UELEWA JUU YA MASUALA YA KIMAENDELEO** 36
- **Hatua ya sita: MAANDALIZI YA UWASILISHAJI** 44
- **Hatua ya saba: ONYESHO** 52
- **Hatua ya nane: UFUATILIAJI NA MPANGO ENDELEVU** 58

**SHUKRANI** 62

# UTANGULIZI

Cre8 East Africa – "cre8" kwa ufupi ni shirika la Kiholanzi linalotumia njia za kibunifu za kisanii kuhamasisha vijana wanaoishi katika mazingira magumu Afrika Mashariki kubainisha changamoto zinazowakumba na kutafuta namna ya kuzitatua changamoto hizo. Nguvu ya Cre8 ipo katika kuunganisha watu ambao watawezesha kuendeleza ujuzi kwenye jamii ziishizo katika mazingira magumu katika ngazi ya chini kabisa kwenye jamii. Cre8 inalenga kwenye vipaji vilivyopo na uwezo wa vijana kuwezesha ujumuishwaji na ushirikishwaji katika kujifunza, kubadilishana uzoefu na kutatua matatizo kwa pamoja.

Cre8 inawawezesha vijana kupitia mashirika ya kwenye jamii zao na vikundi, kuwajengea uwezo wa kubeba na kuongoza jukumu la sanaa ya ubunifu na maendeleo ya jamii ambayo wanapaswa kuyatekeleza, wakati wakiendelea kuyatatua matatizo ya jamii kupitia sanaa. Cre8 pia ianwajengea vijana mshikamano baina yao. Jambo la msingi kabisa, inatoa fursa kwa vijana kupata nafasi na jukwaa juu ya kipi wafanye na kugundua uwezo wao.

Cre8 inafanya kazi kimuundo pamoja na YADEN (Youth, Arts Development & Entrepreneurship Network) Ni shirika lililojikita mjini Nairobi, Kenya linalo fanya kazi Afrika Mashariki kuwasaidia vijana kugundua uwezo wao na kuuendeleza uwezo huo kuwa ujuzi ambao utawasaidia kuishi maisha bora. Kwa njia hiyo, YADEN inawajengea vijana uwezo wa kushiriki kikamilifu kwenye maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.
Ushirikiano kati ya Cre8 na Yaden pia ulihusisha wadau wengine kwa ,miaka kadhaa. Wadau hawo ni kama:

- **Dunga Kenya Development Organisation** in Kisumu, Kenya
- **Marenyo Friends of the Poor Community Support Group** in Yala, Kenya
- **Mkombozi** in Moshi na Arusha, Tanzania
- **Gulu Theatre Artists**, **Amuru Youth Association (AYA)**, **War Affected Youth Association (WAYA)**, **Breakdance Project Uganda (BPU)** na shule ya msingi ya bweni ya **Laroo kwa watoto walioathirika na vita pamoja** na **SOS Children's Village** ya Gulu, Uganda.

Kwenye kila mradi ambao Cre8 na YADEN wamefanya pamoja, wamekuwa wakitumia ubunifu, ugunduzi na ujumuishwaji na ushirikishwaji wa hali ya juu kwa vijana ambao ulikuja kujulikana kama mkakati wa "Cre8 in 8". Kati ya mwaka 2006 na mwaka 2012, njia hii ilitumika kwenye miradi sita ikiwahusisha vijana waishio kwenye mazingira magumu, Kenya, Tanzania na Uganda.

1. **Luanda miradi wa Dunga "Okang Machielo"**, kwa mradi ujulikanao kama hatua inayofuata (The next step) Dunga Beach Kisumu, Kenya (2006). Mradi huu ulijumuisha watoto 150 kutoka shule isiyo rasmi ya Dunga na ilihusisha mada ya usafi na afya kwa ujumla.
2. **Ngimana Mabiro**, "Maisha yangu, Matarajio yangu" ukijikita mjini Yala, Kenya (2007). Mradi huu ulihusisha vijana 60 na ulikua unalenga kutambua fursa za kimaisha.
3. **Jukwaa la vipaji** (house of talents) Moshi, Tanzania (2009). Mradi huu ulijumuisha vijana 40 waishio katika kituo cha watoto cha Mkombozi pamoja na vijana 15 kutoka kwenye jamii. Lengo kuu ilikua ni kuwawezesha vijana kupambana na changamoto wanazokumbana nazo na kutumia vipaji walivyonavyo kuleta mabadiliko.
4. **AMKA** (Rise up) Moshi, Tanzania ikihusisha ziara ya Bagamoyo, Dar es Salaam na Arusha kwa Tanzania pamoja na Nairobi, Kisumu an Nakuru kwa Kenya (2010). Mradi huu ulijumuisha vijana 40 kutoka mkombozi na wengine 15 kutoka kwenye jamii. **AMKA** ilihusu maisha ya watoto wa mitaani, adha wanazopata na vurugu wanazokumbana nazo na tumaini lao la kuwa na maisha bora.
5. **Kati Atyer** "awo kimia" Gulu, Uganda Kaskazini (2011). Mradi huu ulijumuisha vijana 55 na viongozi 6 wa makundi. Lengo la kwanza lilikua ni kuchunguza athari za kila mmoja za vita, halafu kushirikishana na kutatua athari hizo. Lengo la pili ni kuwafundisha viongozi wa makundi kwa kutumia njia ya "Cre8 in 8"
6. **Gulu Youth Festival**, Uganda Kaskazini (2012). Mradi huu ulihusisha washiriki kutoka makundi sita ya Kati Atyer pamoja na vijana wengine 200. Lengo ni kuwashirikisha vijana wote kwenye matamasha na kuhamasisha majadiliano ya wazi juu ya athari za vita na hatua za kutatua matatizo yanayowakabili.

Ufuatiliaji na tathmini kwa kila mradi ulionesha kuwa miradi yote ilifanikiwa kikamilifu. Mafanikio haya yakachochea timu ya Cre8 Afrika Mashariki kuandika uzoefu huo kwenye mwongozo huu, "Cre8 in 8" mkakati huu wa "cre8 in 8" unatoa kitabu cha vitendo kusaidia na kuwezesha watu wanaofanya kazi na vijana kwenye maeneo ya sanaa ya ubunifu na maendeleo ya jamii.

# KUTAMBULISHA MKAKATI WA “CRE8 IN 8”

“cre8 in 8” imejikita katika misingi mitano:

1. Kukuza ujumuishwaji na ushirikishwaji
2. Kutambua na kuendeleza vipaji
3. Kukuza ushirikiano na kubadilishana uzoefu
4. Kuonyesha kuwakubali na kuwaheshimu watoto na vijana
5. Kuhamasisha kila mtu na kuwa na sauti ya pamoja.

Sanaa na kila kipengele chake, ni ukuzaji wa maisha na inahakisi na kuwakilisha namna tunavyoishi ambapo inaonesha tumaini letu, wasiwasi na ndoto zetu. Ni kwa sababu hii ambapo hatua nane zinazo fungamana za “cre8 in 8” zilipelekea kuanzishwa. Kutambua kwa undani hatua moja kutawezesha kufanikisha hatua inayofuata. Mafanikio ya kila njia kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo:

- Uelewa madhubuti wa washirika (wadau) na washiriki wa njia na mbinu hiyo.
- Kujituma, shauku na nia ya kila mmoja anayehusika.
- Uwekezaji madhubuti wa muda na uwepo wa kila mmoja.
- Uwazi na uhamasishaji wa uhuru wa kujieleza.
- Heshima kwa kila anayehusika.
- Uwezo na utayari wa kila mmoja kufanya kazi kwa namna awezavyo na kadri ya uwezo wake

Hatua nane za Makati wa “cre8 in 8” ni:

**1. Kuandaa na kuanzisha mradi**
**2. Kuhamasisha washiriki**
**3. Kuunda kundi**
**4. Kuchunguza na kugundua muonekano wa kisanaa**
**5. Kuchochea/kuendeleza uelewa wa mambo**
**6. Kuandaa taarifa na utendaji (kuandaa sanaa)**
**7. Kufanya sanaa/onyesho**
**8. Kupanga ufuatiliaji kuhakikisha matokeo chanya/ yaliyokusudiwa**





Njia hii inalenga kusaidia makundi ya vijana, mashirika ya kijamii au watu kutengeneza miradi yao. Inalenga kwenye:

- Kugundua vipaji na kuendeleza ujuzi wa Kisanaa.
- Kutoa mafunzo ya stadi za maisha, ikijumuisha kujiheshimu na kujiamini pamoja na kujenga uwezo wa kujieleza.
- Kutambua changamoto kwenye maendeleo na kuzitatua.
- Kutoa mafunzo mahususi juu ya jambo fulani huku tukiangazia changamoto zinazokwamisha maendeleo zinazojitokeza.
- Kukuza ushiriki wa jamii
- Kuwezesha matokeo ya muda mfupi na muda mrefu ya ufuatiliaji pamoja na tathmini na uandaaji wa taarifa.

Mkakati wa “Cre8 in 8” pia unahamasisha suala la upatikanaji wa vifaa na kazi za kujitolea kutoka kwenye jamii husika, badala ya kutegemea masaada kutoka nje ya jaamii hyo. .

**Mkakati wa “Cre8 in 8”: Hatua kwa hatua**







# HATUA YA KWANZA:
## MAANDALIZI NA UANZILISHAJI

Cre8 in 8

*kushindwa kupanga ni kupanga kushindwa.*

## UTANGULIZI

**Hatua ya kwanza inaunda msingi wa kutoa nafasi kwa Waanzilishi wa mradi kujadili mawazo na wadau. Hatua hii ni kama kujaza mawazo kwenye boksi. Kila mmoja anakaribisha mawazo akiwa na utayari kifikra. Dhahiri, ni muhimu kutokufanya hitimisho juu ya jambo na mawazo kwenye hatua hii kwa hatari ya kuwa mkali sana na kupuuza au kukata tamaa.**

### YALIYOMO NA MIONGOZO

Kwenye hatua ya kwanza, **wazo la mradi** linaanzishwa. Hili ni jukumu la mwanzilishaji au waanzilishaji wa mradi. Mawazo kwa kiasi kikubwa yanatoka kwa watu/washiriki. Hata baada ya kuchangia kwenye kundi, wazo litaendelea kurejelewa/kupitiwa kutoka kwa mtoa wazo. Kama una wazo, unaweza kuangalia sehemu iliyo tulia ili kulipambanua wazo lako peke yako. Sasa unaweza kuandaa pendekezo la mradi iwe kwa maneno au vinginevyo (mfano kuchora)- kuwasilisha wazo lako kwa wengine. Kulingana na pendekezo la mradi, unaweza pia kuwashirikisha watu wengine juu ya wazo lako.
Unaweza kupata msukumo kwa kusoma vitabu au magazeti, kutizama video au kusikiliza muziki unaohusiana na wazo lako. Unaweza pia kutembelea sehemu za makumbusho au za kihistoria au pia kutembelea sehemu yoyote ya kujifunza kijijini kwako au mjini- chochote kitakachoweza kuliboresha wazo lako na kulifanya liwe lenye faida kwa mazingira husika.

### 'WAZO LANGU LINAKUWA WAZO LETU'


Kuuunda wazo la mradi kunaanza kutoka kwenye watu wenyewe kupendekeza mawazo binafsi na wengine kupewa nafasi ya kuchangia mawazo hayo ambapo hii itabadili wazo hilo la mtu kuwa wazo la kundi. Kwenye mchakato, wazo lililopendekezwa na mshiriki linaweza kubadilika na kuwa tofauti kabisa. Hamasisha kila mshiriki kushirikishana mawazo yao na kila mmoja, maana kwa kufanya hivi itapaelekea kupata wazo lililojitosheleza la mradi. Pia unapofanya kazi na washirika wengine ni muhimu pia kuwahusisha kutoa wazo au kuchangia.

Inashauriwa kurekodi na kuhifadhi taarifa zote zihusianazo na mradi zilizokusanywa, kwa mfano kwenye **sanduku la mradi**. Sambaba na **ufuatiliaji na tathmini**, inashauriwa pia kuandaa taarifa zozote zipatikanazo kutoka kwa washiriki au mshiriki ikiwemo matarajio yake binafsi. (kielelezo cha boksi la mradi)




Baada ya wazo la mradi kukamilika, wewe kama mwanzilishi unapaswa kuweka **mpango wa mradi**. Hii inajumuisha orodha ya vitu vinavyopaswa kujumuishwa na mawazo yanayopaswa kutolewa ili kuupangilia maradi:


- Mradi utafanyika wapi?
- Nani atahusika katika mpangilio na kusaidia mradi?
- Rasilimali gani zinahitajika na ni nani ata shughulikia? Rasilimali fedha na rasilimali vitu kwa mfano sehemu ya mazoezi vinaweza kupatikana bure kutoka kanisani, msikitini, shuleni, kutoka kwenye jamii n.k?
- Nani atasimamia kipi (mfano kiongozi wa sanaa, msimamizi, na meneja wa fedha)? Kuhamasisha mgawanyo wa majukumu kama jukumu la mahusiano ya jamii (kufanywa na msimamizi). Mbinu hapa ni mgawanyo wa majukumu na vifaa kuepuka migongano na malimbikizo ya majukumu kuhakikisha kunakuwa na mgawanyo mzuri kati ya kazi na utaratibu wa taarifa
- Watu gani watashiriki (watoto, vijana. N.k) na kwa vipi watachaguliwa?
- Nani watakuwa walimu wawezeshaji na Nyanja zao za kisanaa?
- Vifaa gani vya mazoezi  vitahitajika na ratiba nzima ya mazoezi?




## MFANO

Mwaka 2004, mratibu wa mradi wa Cre8 alikwenda Dunga beach, nje kidogo ya Kisumu, Kenya. Hapa wazo la mradi na mpango mradi vilipatikana kutokana na uchunguzi binafsi kutoka kwenye majadiliano na watoto, na kutokana na mahojiano na walimu wao, na mashirika ya maendeleo ya vijijini. Matokeo yake Cre8 waliandaa mradi wa onesho la watoto ambalo:

- Lilijikita zaidi kwenye taarifa na msukumo kutoka kwa watoto ambao walifanya kazi na mratibu.
- Lilishughulikia Afya na usafi, kwani watoto wengi walikua wakiumwa mara kadhaa kwa sababu ya uchafu na hali ya mazingira.
- Lilijikita katika kutambua, kuendeleza na kutoa fursa kwa vipaji vya kisanii.



Luanda miradi wa Dunga "Okang Machielo", kundi la watoto walipewa kazi ya kuzunguka kijijini na karatasi na kalamu kuchora vitu. Mwisho wa siku wote wakarejea na kushirikishana mawazo yao. Mvulana mmoja alichora picha tatu; moja ilionesha watu wanakata miti, nyingine ilionesha mtoto anaomba chakula huku akilia, na ya tatu ikionesha polisi wakiwakamata watu wanaokata miti. Kwa msingi wa picha hizi, kundi la ngoma baadae liliweza kuandaa ngoma.

Kwa Yala, timu ya Cre8 ilitembelea Kijiji cha Marenyo na kukaa chini na vijana wadogo pale kijijini ambao walitoa mawazo juu ya mradi. Mawazo yote yaljadiliwa mezani na mawazo makuu yaliteuliwa kuandaa wazo la mradi, ambalo baadae lilipelekea kuwepo kwa mpango mradi.



Cre8 inahamasisha wadhamini wa ndani ya jamii kama Makanisa, Misikiti, Vituo vya kijamii, Familia na Marafiki. Kama una shirika lililo tayari limeanzishwa, unaweza kuomba masaada wa vitu na fedha kutoka kwa wanachama au pia kutoka kwa ndugu nakadhalika. Cre8 pia inajenga kundi la mradi, linalohusisha wanachama kutoka mashirika yanayofanya nao kazi (tumia tovuti kuchunguza namna ya kukusanya fedha au vitu na chagua moja ambayo ni sahihi kwako, tumia maneno kama, "Mpango wa kuchangia makundi ya vijana", au "mpango wa kuchangia kwa miradi ya kisanaa ya kijamii nakadhalika kutafuta msaada).

Mwisho wa hatua ya kwanza, timu ya uanzilishi wataandaa kwa pamoja MPANGO MRADI. Hii itasaidia kutoa muongozo kwa timu na pia kutumika kuandika pendekezo kwa wafadhili. Hii ni pale ambapo UFUATILIAJI NA TATHMINI vinapoandaliwa na kukubalika.

## HITIMISHO

Hatua ya kwanza ni pale unapoendeleza wazo kuwa mpango mradi wenye faida. Husisha wadau wengi kwenye hatua hii kwanzia mwanzo na kubali kupokea mawazo na mapendekezo yao. Wahusishe kwenye utekelezaji wa mradi kwanzia mwanzo pia. kwa njia hii, wazo lako kwa ajili ya mradi litaungwa mkono na kundi kubwa au jamii.

## VITU VYA KUZINGATIA KABLA YA KWENDA HATUA INAYOFUATA

**Mpango mradi unahusisha:**

- **Malengo ya mradi**
- **Matokeo yatarajiwayo**
- **Kundi lengwa/ walengwa**
- **Wafadhili**
- **Sehemu ya mradi**
- **Muda wa mradi**
- **Kipindi cha mradi**
- **Maelezo juu ya bajeti na rasilimali zilizopo**
- **Ubunifu wa kisanii unaolengwa/nidhamu**
- **Majina ya timu nzima ya mradi (wanachama)**
- **Mpango mahususi wa namna mradi utakavyoedeshwa, kutathminiwa na kutolewa taarifa.**
- **Mpango endelevu**



# HATUA YA PILI:
## UHAMASISHAJI WA WASHIRIKI

Cre8 in 8

*Pamoja tunaweza*

## UTANGULIZI

**Uhamasishaji unahusisha kutambua na kuwaleta washiriki wa mradi pamoja kwa mijadala ulioifanya kwenye hatua ya awali (hatua ya kwanza). Kama una mpango wa kufanya kazi na mashirika mengine rafiki hakikisha unawahusisha kwenye mchakato mapema iwezekanavyo. Kwa mfano, kama unahitaji kundi kubwa la washiriki unaweza kufanya kazi ukisaidiana na taasisi mbalimbali za elemu, mashirika ya maendeleo au taasisi za kidini ambao watakusaidia kugundua washiriki wanaostahili kushiriki kwenye mradi**

### YALIYOMO NA MIONGOZO

Rasilimali kuu katika mradi wowote ule ni WATU. Hii inajumuisha:

1. Mwanzilishi/waanzilishi wa mradi
2. Timu ya mradi
3. Kundi linaloshiriki (washiriki)

Vigezo vya kuzingatia wakati wa kuchagua washirika wakufanya nao kazi:

- Wana msingi madhubuti?
- Wana moyo wa kusaidia vijana/watoto na jamii?
- Wanaweza kusaidia upatikanaji wa rasililimali kama sehemu, wawezeshaji wenye ujuzi na wasaidizi (wapishi, usafiri n.k)?
- Wana uzoefu wa kutosha katika kiwango chochote?

Chagua timu ya kufanya nao mradi kwa kuzingatia yafuatayo:

- Kwa kuzingatia maslahi yao na shauku yao
- Uwezo wao wa kutumia ubunifu wa kisanii/ nidhamu ya mabadiliko katika jamii (au utayari wa kujifunza namna ya kufanya hivyo)
- Uwezo wa kuelekeza/kuongoza/kufanya maamuzi
- Upatikanaji wao
- Namna wanavyoweza kubadilika kulingana na hali halisi.
- Vipaji vyao na ujuzi wao walioonyesha katika fani zao
- Mapendekezo kuhusu utendaji wao kutoka kwa washirika na wadau wengine
- Wasifu wao (C.V) kwa maandishi, mdomo, video n.k.






Unaweza kuomba mashirika wanachama kupendekeza wanachama wenye uwezo, inapendekezwa wapatikane kwa mchakato wa kidemokrasia.

**1. Waanzilishi wa mradi**
Waanzilishi wa mradi wanaweza kuwa mmoja au zaidi au hata pia mashirika (kama kuna ushirikiano).

**2. Timu ya mradi**
Timu ya mradi inahusisha watu waliopatikana kutoka mashirika washirika na wanakuwa na jukumu la utekelezaji wa mradi. Kutokana na mahitaji ya mradi, wanachama wanaweza kuwa na majukumu kama kiongozi wa sanaa, msimamizi au mratibu, meneja wa fedha, meneja mahusiano au meneja wa mawasiliano, na mwezeshaji wa ujuzi. Idadi kamili na waliomo kwenye mradi hutegemea na mahitaji ya mradi husika, ukubwa wa mradi (ikijumuisha na idadi ya washiriki) na upatikanaji wa wanachama. Kwa vile wanachama wengi wa mradi watahusika tu kwenye hatua ya pili hivyo wanapaswa kupewa taarifa kwa ufupi juu ya nini, wapi, lini, kwa nini na kwa vipi mpango mradi ni muhimu.

Chagua washiriki kwa kuzingatia:

- Upatikanaji (kwa kuzingatia muda)
- Ubunifu wa kisanii/ nidhamu
- Shauku, kipaji na nia anayoonyesha
- Uanachama au mshikamano na uelewa wa kundi legwa
- Uelewa wa mradi na malengo yake
- Matarajio yake
- Umri
- Mapendekezo kutoka kwenye jamii au mashirika juu ya mtu anayefaa kushiriki.



Ni muhimu kukusanya taarifa za msingi (kwenye chanzo halisi) kwa kila mwanachama (tazama hapa chini) unaweza kutumia jedwali kama lifuatalo kuandika taarifa za kila mwanachama.

**3. Kundi la washiriki**

Vijana au watoto ni wanufaika wakuu wa mradi. Ni wangapi watahusika, itategemea kwa kiasi kikubwa rasilimali zilizopo, maslahi na mahitaji yaliyoelekezwa kwenye Mpango mradi. Vigezo vifuatavyo vinapaswa kuzingatia kwenye upatikaaji wa kundi la washiriki:

- Washiriki lazima watoke kwenye jamii ile.
- Washiriki lazima wateuliwe kupitia mchakato unaozingatia usawa wa Kijinsia, hali ya kimaisha, nidhamu ya kipaji, maslahi ya jamii n.k.
- Malengo ya ushiriki lazima yabainishwe.
- Likizo za shule na ratiba nyingine za kijamii lazima zizingatiwe ili kuhakikisha upatikanaji wa washiriki.

**TAARIFA ZA MSINGI ZA TIMU NZIMA**

| NA. | JINA | JINSIA | UMRI | MAWASILIANO | SHIRIKA | KAZI/NAFASI | NIDHAMU YA KISANII | MAELEZO YA ZIADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | | |



**TAARIFA ZA MSINGI ZA WASHIRIKI**

| NA. | JINA | JINSIA | UMRI | MAWASILIANO | KUNDI/ SHIRIKA | NIDHAMU YA KISANII | ANASOMA (NDIO, KIWANGO GANI) HASOMI | MAELEZO MENGINE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | | |

Ni muhimu kufanya ukaguzi wa washiriki wakati wa usajili. Hii itajumuisha ukusanyaji wa taarifa za misingi kwa vitu kama umri, jinsia, maslahi, mawasiliano, kwa kila mshiriki na pia kwa mzazi wake, walezi au kundi la vijana, kiwango cha elimu, kama anasoma au hasomi, na lugha yake ya mawasiliano.

Orodhesha washiriki wa mradi kwa kutumia jedwali kama linaloonekana hapo juu.

Kumbuka kwamba ni muhimu washirika utakao wachagua na kufanya nao kazi wawe na asili/ hali inayokaribiana kwa kiasi kikubwa. Hii itasaidia kujenga mshikano ndani ya kundi (ambayo pia itachangia matokeo chanya). Kwa mradi wa muda mfupi kama huu kutakua na muda mdogo wa kutambua changamoto kubwa za kwenye kundi.

Kwa upande mwingine, ni muhimu kwenye kundi mshiriki kuwa na vigezo tofauti tofauti kama, nguvu yao, uwezo wa kisanaa, maslahi yao n.k ili



kuhakisha timu iliyo jizatiti na yenye usawa.

Linapokuja suala la kuchagua washiriki, unaweza kuwa na washirika wako na kuwagawa kwa kuzingatia vigezo vilivyobainishwa au unaweza kufanya  mchujo.

### MFANO

Kwa Gulu, Cre8 waliwawezesha YADEN, ambao walifanya upembuzi yakinifu juu ya mradi. Kuptia tafiti hii, na kutokana na msaada kutoka kwa Quinto Okello, Mratibu wa mtandao wa YADEN, wanachama wawili (2) wa Cre8 walitembelea Gulu na kuongea na mashirika wanayofanya nayo kazi. Ziara hii ili wawezesha kuapata washirika wawili waliokuwa tayari kufanyanao kazi ambao walikuwa ni kundi la vijana la AYA, kikundi cha sanaa cha Gulu, kundi la vijana la Waya (Waya youth group) na mradi wa Breakdance Uganda,



na pia shule ya msingi ya bweni ya Laroo kwa watoto walio athirika kwa vita, na kiongozi wa kundi/mwezeshaji. War child Uganda pia walituma wanafunzi na chuo cha Gulu walituma wanafunzi wawili. Kwa idadi ya majina 70, ukijumuisha na wakufunzi 10 wa Cre8, idadi ya washiriki wa mradi ikakamilika.

### HITIMISHO

Usipofanya mradi na makundi ya awali, hatua ya pili (2) (kuchagua timu ya mradi na kukusanya washiriki wa kundi) itakuwa ni muhimu lakini itakuwa ni mchakato utakao tumia muda mwingi. Ni muhimu kuwekeza kwenye hatua hii kwa sababu mafanikio ya mradi wako yatategemea hatua hii. Japo Cr8 wanatilia mkazo umuhimu wa ujumuishwaji wa watu kwenye mradi,inatambua pia haja ya kuchagua washiriki, kwa sababu kuna muda mfupi kubaini tofauti kubwa za washiriki au makundi madogomadogo (labda tofauti hizo zitokee mwanzo na kuwekwa sawa kama moja ya mchakato).

Kwa kigezo hicho, Cre8 kila mara wana pendekeza kufanya kazi na wadau/washirika wa maeneo husika ambao wanaweza kugundua washiriki wanaofaa. Cre8 kwa kawaida wanafanya kazi na makundi yenye kati ya watoto au vijana (washiriki) 50 mpaka 60.

## MAMBO YA KUZINGATIA KABLA YA HATUA INAYOFUATA

- **Orodha ya washirika wako, pamoja na kazi zao husika na majukumu yao.**
- **Orodha ya wakufunzi wa sanaa/ timu ya wanachama wa mradi pamoja na taarifa zao za mawasiliano au kazi, majukum, na wajibu wa kila mmoja.**
- **Orodha ya washiriki sambamba na taarifa zao za msingi (jina, umri, jinsia n.k) pamoja na mawasiliano yao.**



# HATUA YA TATU:
## KUJENGA KUNDI

Cre8 in 8

*Wote tuko katika uelekeo sawa?*

## UTANGULIZI

**Kuunda kundi ni mchakato wa mara kwa mara na endelevu bila hivyo ufanisi wa matokeo ya mwisho utatiwa dosari. Hata kama unafanya mradi na kundi la wahusika ambao tayari wanafahamiana, ni muhimu sana kuendeleza mchakato wa kujenga kundi kwa sababu kila mradi una mambo mapya. Waweza kujikita kwenye baadhi ya vigezo kama kutambua ujuzi wa kila mmoja, asili na kipaji kwa kila mmoja.**

### YALIYOMO NA MIONGOZO

Hatua ya kutengeneza kundi inahusisha michakato kadhaa:

**1. Kujiridhisha na kila mmoja na kufanya utambulisho**

Kutambulisha mradi na kutambulisha timu nzima ya mradi.
Andaa kikao kwa washiriki wote (ukijumuisha timu ya mradi). Kuna baadhi ya watu watakuwa wanafahamiana lakini pia kuna wengine watakua wanaonana kwa mara ya kwanza. Tambulisha kila mtu kwenye timu ya uwezeshaji wa mradi na majukumu yao. Mkutano huo utakua na umuhimu kutambulisha kwa mara nyingine malengo ya mradi, ratiba/utaratibu na mipango ya dunia. Japo watu wengi watakua tayari wamekwisha sikia kabla, itakuwa tofauti na kwa kiasi fulani "yenye uhalisia" kama itafanyika kwa mara ya kwanza na kila mmoja akiwemo.
Kwa hatua hii, ni muhimu kuweka dira kwenye mradi kwa kuwalenga walengwa wakwanza wa mradi kuhakikisha wanatambua kuwa mradi ni jukumu lao na sio kitu ambacho wanapaswa kufanyiwa.

Angalizo, epuka maneno mengi, lenga hasa maneno machache yenye hamasa. Kama inawezekana epuka mjadala mrefu kwa kila jambo unaloona limeenda vibaya. Mijadala hiyo inaweza kusambaratisha kundi hata kabla halijaimarika. Wakati huo huo epuka kuziweka bayana tofauti za washiriki (mfano, maeneo watakayo, vipaji vyao kisanaa, umri n,k) katika hatua za mwanzoni za uandaaji wa kundi, lakini badala yake tilia mkazo katika mfanano wao na malengo yao kiujumla.

Ni muhimu kuchunguza uhusiano chanya baina ya waanzilishi, timu ya mradi (wafanyakazi) na washiriki. Kwa mradi wa kijamii, mahusiano, mshikamano, na kuaminiana (imani) kati ya washiriki wa mradi kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuleta mafanikio.

*Kuwatambulisha washiriki*
Baada ya timu ya mradi (wafanyakazi) kujitambulisha na kutoa maelezo kwenye kundi juu ya mradi, hakikisha kila mshiriki anapata nafasi ya kujitambulisha vizuri, iwe kwa kifupi kujitambuslisha jina na maelezo mengine ya ziada anayojisikia kueleza (mfano, kundi analoliwakilisha, umri wake, kipaji chake n.k) au kwa kuwatambulisha.
Kama hali ya kiusalama itakua ya mashaka basi ni vyema suala la utambulisho ukawauliza washiriki kwanza. Pia waweza kuwapa fursa washiriki kujitambulisha wenyewe wakiwa na wanakikundi wenzao. Kila unachokifaya hakikisha unazingatia kanuni na taratibu za sehemu husika.

**2. Kufahamiana. Namna ya kufanya**

Kuna njia nyingi za kuwafanya washiriki kufahamiana. Kwa mfano unaweza ukawakusanya watu wote kwenye duara, halafu ukaanza na zoezi rahisi kama zoezi la kunyoosha viungo au mchezo wa kujuana majina. Hatua kwa hatua, unaweza kuanzisha michezo na mazoezi mengi yahusuyo kujuana majina. Hakikisha inakua ni michezo na mazoezi mafupi yenye kufurahisha. Mwezeshaji anaweza kuongoza mwanzoni, lakini kadri hali inavyokua vizuri baina ya washiriki/wanakikundi, hamasisha washiriki kuongoza mazoezi. Pamoja na mazoezi ya viungo, yatawafanya washiriki kujiachia na kuwa huru.

Vilevile pamoja na michezo ya kisanaa itawahamasisha washiriki kujieleza (na kuonyesha vipaji vyao kwa wengine wakati wa mchakato huo).
Mchakato wa kufahamiana unaweza kuchukua siku chache mpaka wiki kadha, lakini washiriki kwa kawaida lazima lazima waanze kuzoeana siku za mwanzoni za mradi (zoezi). Katika mchakato, mwezeshaji pia atapata maelezo/ ufahamu juu ya tabia na historia za kila mshiriki.

**3. Kujenga mahusiano chanya baina ya washiriki**

Baada ya zoezi ni muhimu kuhamasisha kundi kuulizana maswali na kupeana majibu sahihi. Hamasisha washiriki kushirikisha mawazo yao kwenye mazoezi na michezo. Hii itawasaidia kujengeana imani. Mwezeshaji anaweza kuwapa washiriki watatu jukumu la kuongoza mazoezi na siku zinazofuata kuwaomba washiriki hao kuandaa somo kwa pamoja.

### MFANO

Katika miradi ya **Jukwa la Vipaji** na **AMKA** (Mkombozi, Moshi), washiriki wote, wafanyakazi wa shirika la Mkombozi , timu ya Cre8 na walimu wa sanaa wa Moshi kwa pamoja walijumuika kwenye ukumbi mkuu. Baada ya neno la ukaribisho kutoka kwa Simon (Mwalimu wa michezo Mkombozi), Mratibu wa mradi wa Cre8, Ben alielezea malengo ya mradi na kwa ufupi alielezea nini maana ya Cre8, kipi walikifanya siku za nyuma na kwa nini wamechagua kufanya kazi na Mkombozi.

Walimu wa sanaa mbalimbali walipewa nafasi ya kujitambulisha lakini badala ya mbinu ya kujitambulisha kwa kuanza na "jina langu ni…." Walijitambulisha kupitia sanaa zao. Diana, mwalimu wa kucheza ngoma alijitambulisha kwa kucheza ngoma ya asili, wakati mwalimu wa sarakasi Eddy, alijitambulisha kwa kuonyesha sarakasi chache. Harrison, mwalimu wa muziki, aliongoza kundi zima kuimba kama kiitikio. Hii ilihamasisha washiriki kuja mbele na kuonyesha baadhi ya vipaji vyao pia, ambayo kwa kiasi kikubwa ilipelekea siku ya utambulishi kuwa ya furaha sana.
Sami, mwezeshaji wa sanaa na maendeleo, aliongoza washiriki kushirikishana matarajio yao na kutoa mawazo yao juu ya Mpango Mradi. Washiriki walikuwa huru na wazi kujieleza baada ya utambulisho ule pengine hata zaidi ya ambavyo tungefanya utambulisho wa kawaida.

### HITIMISHO

Mkusanyiko wa kwanza ni wa muhimu sana katika kujenga mshikamano kwenye kundi, japo utangenezaji wa kundi ni mchakato ambao unaenda mpaka mwisho wa mradi tena wakati mwingine unaenda mbali zaidi. Kwenye hatua hii, lengo ni kuwezesha kuwa na mwanzo mzuri, ambao kila mmoja anajisikia amethaminiwa na kujumuishwa. Ni muhimu kutambua kuwa shughuli rasmi na zisizo rasmi za ujengaji wa kundi zinazingatiwa kwenye kila hatua ya mradi.





## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA HAPA

- **Kila mshiriki kutambua mradi, malengo yake na matokeo yatarajiwayo. Hili linaweza kuthibitika katika namna watakavyoweza kujibu maswali au kwa kupitia majadiliano.**

- **Washiriki wote kujisikia huru, wazi na pasipo kuwa na wasiwasi. Hii inaweza kuthibitika katika namna wanavyoshirikiana, ushiriki wao katika michezo na ushirikiano wao kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.**

- **Kundi linafanya kazi kama timu. Hili linaweza kuthibitika kwa kigezo kuwa washiriki wana tekeleza majukumu yao, wanazingatia muda wao kikamilifu na wanachukua hatua kwa kupendekeza mawazo n.k.**



# HATUA YA NNE:


## UCHUNGUZI WA KISANAA NA UGUNDUZI

Cre8 in 8

*Kuonyesha kipaji*

## UTANGULIZI

**Wakati wa utangulizi, walimu wa sanaa wanatambulisha vipaji vyao (sarakasi, maigizo, ngoma n.k) kwa njia ya kibunifu zaidi ambayo washiriki watahamasika na kushawishika na namna ambayo si ya kuhatarisha au kuwatisha. Baadhi ya vijana wadogo wanaweza kuogopa na kuonea aibu baadhi ya mambo mapya kama vile sarakasi, mazingaombwe au ngoma za kisasa. Wanaamini kuwa itakuwa ni vigumu na hatari kufanya. Utangulizi wa wa mwalimu aliebobea juu ya ubunifu, kuwaalika na kuhamasisha vijana hao itasaidia kuinua hamasa zao kuondoa aibu zao au uoga. Kazi kuu ya Mwalimu wa sanaa ni kuwashirikisha wasanii sanaa aifanyayo ambayo itawapa changamooto na nafasi ya kujifunza na kuiweza ndani ya muda lengwa. Hakuna kinachotia hamasa zaidi kama kupata matokeo chanya. Baada ya kupita katika hatua ya 3, ambapo washiriki walihimizwa kuwa huru na kujenga kujiamini na kila mmoja, washiriki watakua wameandaliwa ku "thubutu".**



### YALIYOMO NA MIONGOZO

**Soko la vipaji**

Gawa wanakikundi katika vikundi vidogo vidogo kulingana na idadi ya sanaa zilizopo au zilizolengwa. Tengeneza ratiba pamoja na kuwapa fursa washiriki kuchagua mmoja kati yao kuwa kiongozi wa kikundi hicho kidogo. Majukumu ya kiongozi wa kikundi ni kuhakikisha muda unafuatwa na nia pia kuwa kiungo kati ya mwalimu wa sanaa na washiriki. Kila mwalimu ana sehemu yake ya kufanyia kazi, na kila kikundi kinapata mafunzo kwenye kila sanaa.

Unaweza kuwa na kipindi cha dakika 60 kwenye kila kundi kwa mzunguko au (mbadilishano) wa masaa matatu wa nusu siku, kutegemeana na muda wa mradi. Ifanye iwe fupi ili kuwafanya wawe na umahiri na kuendeleza hamasa za washiriki lakini pia iwe ndefu kupelekea kupata matokeo yanayoonekana. Kama unachagua mbinu ya kuwa na nusu siku na kwa mfano una sanaa tofauti tano (5) (Ngoma, muziki uchoraji, sarakasi na maigizo) utapaswa kuwa na nusu siku mbili. Kwa namna hiyo, unaweza kutumia muda wa mchana kwa tafakari ya siku, ikijumuisha uwasilishaji na uundaji wa makundi yakisanaa ya kudumu. Hiki ndo ambacho Cr8 wanakiita "soko la vipaji".

Baada ya kila mmoja kupitia kila sanaa, washiriki wanaweza kujiunga na kundi lake la sanaa analopenda. Kwa kuzingatia uchunguzi wao wenyewe na kuzingatia usawa wa kundi, walimu wa sanaa wanaweza kupendekeza mabadiliko pamoja na kuhamisha washiriki kutoka kundi moja kwenda kundi lingine, kutengeneza makundi ya sanaa ya kudumu. Hili linapaswa kufanywa kwa njia ya upole na ya kuvutia. Kwa sababu kama

washiriki wana vipaji zaidi ya kimoja, ni muhimu kuhakikisha wanajiunga na makundi yatakyowapa changamoto mpya au ambapo ujuzi wao juu ya sanaa fulani utahamasisha wengine.

Kama kujenga uwezo kunachukua siku tano, na soko la sanaa linachukua siku tatu, washiriki watapata mafunzo kikamilifu katika siku mbili zilizo baki. Katika hatua hii, mwalimu wa sanaa ataambatanisha taarifa za kila mshiriki kulingana na wakati uliopo na atachukua muda kutoa mawazo juu ya alichogundua kutoka kwa washiriki.

## MFANO

Mradi wa Cre8 unahusika hasa na kujenga uwezo na utoaji mafunzo juu ya mambo ya kisanii na matokeo yake. Cre8 inahitaji kuvumbua vipaji na uwezo wa washiriki katika sehemu iliyo huru na wazi. Vijana wengi wanao jiunga na mradi kwa kawaida wanajua kuwa wana vipaji. Lakini si kila mara inajulikana ni "Kipaji kipi" na ni kwa "namna gani". Kwenye mradi wa Cre8 watapata nafasi ya kutambua uwezo wao. Baadhi ya washiriki watashangaa wenyewe. Kwa Cre8, suala la ugunduzi wa vipaji ni jambo la msingi katika kuboresha uwezeshwaji wa vijana.

Binti wa miaka 17, Quinter alijitokeza katika mradi wa Cr8 "Ngimana Mabiro" Yala Kenya. Kwenye kipindi cha "Soko la vipaji" aligundua ana kipaji cha kuimba na pia kutunga nyimbo. Kabla ya hapo, alijua kuwa anakipaji cha kucheza ngoma, ambacho alikipenda zaidi. Kishingo upande alijiunga na kundi la muziki, lakini mwisho wa mradi, kipaji chake cha kuimba kikawa ni ujuzi (kikaimarika) kwenye tathmini yake alielezea kuwa hili ni badiliko lake kubwa na limemsukuma kujiunga na kwaya ya shule na kwaya ya kanisa pia.

## HITIMISHO

Hatua ya 4: Ugunduzi na utambuzi wa vipaji; inahusu kuanza safari na washiriki. Unapaswa kutumia muda mwingi kwenye hatua hii na kumpa kila mshiriki nafasi sawa bila upendeleo. Hapa ndipo pale ubora wa mwalimu unapojidhihirisha. Mbali na kuwa na uelewa kwenye fani zao, pia unapaswa kutazama mbali zaidi na kuona, kubaini vipaji vilivyofichika.

Mwisho wa hatua hiii, vikundi vya sanaa mbalimbali watakuja pamoja na kuwasilisha kile walichofanya mbele ya makundi mengine; Mkurugenzi wa sanaa atapata fursa na hamasa ya kushuhudia uwasilishwaji huo kwa sababu uwasilishaji huu unaunda baadhi ya vipengele kwa ajili ya kutengeneza onyesho kwa ujumla. Washiriki pia wana pata fursa ya kutoa mrejesho wa kile walichokiona kwa kila mmoja na kutoa mapendekezo na mawazo kwa ajili ya uwezeshaji wa zoezi. Kwenye hatua hii, baadhi ya washiriki wenye uwezo wa kipekee wanaweza kuwa walimu wa ziada na kuongoza kipindi cha mazoezi na washiriki wengine. Baadhi ya vipaji vingi vya walimu wa sanaa vilianzia kwenye hatua kama hii.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA HAPA

- **Washiriki wote wameshagundua fani zao tofauti tofauti.**
- **Walimu wa sanaa wameshagundua vipaji vya kila mshiriki na kuwajuza kila mshiriki amebobea katika kipaji gani.**
- **Kila mshiriki amejichagulia kundi analoona linamfaa.**
- **Washiriki wenye uwezo wa kufundisha wenzao au nia na taaluma ya kufundisha wameshatambuliwa.**



# HATUA YA TANO:

## UELEWA JUU YA MASUALA YA KIMAENDELEO

Cre8 in 8

*Kuelewa changamoto zinazokukabili ni hatua ya kwanza ya kuzitatua.*

## UTANGULIZI

**"sanaa ni maendeleo". Sanaa na kila kipengele chake (muziki, maigizo, uchoraji n.k) ni ukuzaji wa maisha. Inahakisi na kuwakilisha namna tunavyoishi ambapo inaonesha tuumaini letu, wasiwasi na ndoto zetu. Sanaa inatusaidia kuelezea fikra na hisia zetu. Sanaa ni mchakato unaotupa uwezo wa kugundua sisi ni kina nani, zaidi ya hiyo inatusaidia kutupa ramani ya wapi tuendapo na vipi tunapaswa kuwa. "Sanaa si mchakato, ni maendeleo" (Sami Ganthii).**

**Mkakati wa "Cre8 in 8" ni wa kujengeana uwezo unaojumuisha mafunzo ya sanaa na maendeleo ya kila mmoja. Inasemekana kuwa sanaa inaakisi jamii. Kama hivyo ni kweli, sanaa inapaswa kutambua mambo yanayoikabili jamii yake, kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.**

**Hatua ya 5 ya "Cre8 in 8" inatoa muongozo wa kujenga uwezo kwa kuwawezesha kundi lengwa na jamii kubwa kwenye kile kijulikanacho kama mijadala (majadiliano).**

### YALIYOMO NA MIONGOZO

- Tengeneza dodoso ya kwenye mjadala wa kikundi. (tazama mfano hapo chini).
- Chagua msimamizi (mara nyingi awe miongoni mwa timu ya mradi) na mwandishi (maranyingi ni miongoni mwa washiriki, hakikisha wote wanahabarishwa vizuri).
- Kusanya kundi kwa ajili ya majadiliano na hakikisha wote wana kuwa huru na wazi. Inapendendekezwa watu kuwa kwenye duara.
- Fanya mjadala kwenye kikundi.

### Mfano wa mtiririko wa dodoso

*(FDG Focus Group Discussion)*

**1. Vijana wadogo ni wapi?**
Eleza wewe ni nani, kama mwenyewe au kundi. maana ya kijana kwa kawaida inategemeana na umri kwa hali isiyo ya kawaida sana inaweza ikategemeana na sifa nyingine na hali.

**2. Changamoto zao ni zipi?**
Bainisha mambo (changamoto) zinazo wakumba vijana kama zilivyo onekana kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Ni zipi zinaathiri wavulana tu au wasichana tu?

**3. Ni nini kinasabababisha changamoto hizo?**
Fikiri kuhusu sababu za ndani, sababu za nje, sababu za kimazingira, sababu zinazoweza kuzuilika na zisizoweza kuzuilika, nani wa kulaumu n.k


**4. Ni kwa vipi changamoto hizo zinawaathiri?**
Fikiri kuhusu athari za changamoto hizo na ki kivipi zinajitokeza katika maisha ya vijana? Kwa mfano mimba za utotoni zinapelekea msichana kuacha shule n.k

**5. Ni mapendekezo gani yatasaidia kutatua changamoto hizo?**
Fikiria kuhusu suluhiso kulingana na mazingira ya jamii husika. Zingatia kutafuta ufumbuzi (suluhisho) la muda mfupi na ufumbuzi (suluhisho) la muda mrefu, suluhisho lililotokana na mapendekezo ya watu, utatuzi wa kinadharia na vitendo n.k

**6. Vijana wana nafasi gani katika kutatua changamoto hizo?**
Zingatia majukumu ya vijana katika namna ya kuwa sehemu ya kutafuta ufumbuzi kupitia ushiriki hai (Madhubuti).

Mbinu ya Cre8 ya kufanya majadiliano inasaidia washiriki kutathmini juu ya changamoto chanya na hasi zinazowakabili. Msimamizi ambaye anafahamu njia ya majadiliano anatakiwa kuongoza kipindi hicho. Mwandishi anachaguliwa kutoka kwa washiriki ili kuandika mambo yanayojadiliwa.

Mjadala lazima uzingatie mtiririko wa kimantiki ili kuhakikisha washiriki si tu wanabainisha changamoto bali pia wanazichambua kiufasaa na kusaidiana kuzitizama kulingana na mazingira. Kama wanakabiliana na changamoto yoyote wanapaswa kupendekeza suluhisho. Ni muhimu washiriki wakahamasishwa kujadili maoni yao kulingana na uzoefu wao na kujadili mada kulingana na hali halisi ya eneo hilo, kwa mfano ni kivipi kutokuwa na ufanisi kwa serikali kunavyoathiri upatikanaji wa maji kijijini, na kupelekea changamoto mashuleni na matatizo




mengine binafsi. Hii itasaidia kila washiriki kuutizama ulimwengu kwa mtizamo wake. Hii ni kujikimboa na uwezeshwaji kwa maana washiriki wanaanza kujiona kama sehemu ya picha kubwa. Pia ina watia hamasa kuchangia/kujadili hata mambo ambayo awali walidhani hayawahusu hususani pale wanaposhindwa kuhusianisha changamoto za ulimwengu na maisha yao binafsi.

Msimamizi ana himizwa kubadili neno "vijana wadogo" na kuhimiza maneno kama "wewe", na "mimi", "mimi binafsi" au "mimi" ili kuwezesha washiriki kujadili mambo kama wao binafsi (kubeba jukumu). Mbali na mambo mengine, njia/mbinu ya majadiliano inalenga kuwasaidia washiriki:

- Kujitambua wao ni nani binafsi
- Kujiona wenyewe ndani ya jamii kubwa
- Kutizama kwa mapana changamoto zinazowakumba na zinazoikumba jamii yao.
- Kushirikishana na kubadilishana mawazo na uzoefu.
- Kuchukua jukumu la kutafuta mwafaka/ suluhisho.
- Kuwezeshwa, kuwa washiriki hai na kuonyesha jukumu lao kama viongozi kwenye jamii.

*Msimamizi atawahamasisha washiriki kupiga kura kwenye mambo ya msingi kabisa kwenye kila jambo/ changamoto, ambazo ndizo zitakazounda mada/ msingi wa taarifa ya kundi. Kundi litakubaliana juu ya mambo mangapi ya kujumuisha, japokuwa mambo matano kwenye kila kipengele yanatosha. Mambo hayo/ changamoto hizo ndo yataunda msingi wa uwasilishwaji/ onesho la washiriki.*

## KWA MFANO

Mradi wa 'Jukwaa la Vipaji' na 'AMKA', Mkombozi, Moshi Tanzania ililenga kutengeneza jukwaa ambapo washiriki wengi walikuwa watoto wa mitaani, wataweza kushirikisha uzoefu wao na kuhamasisha watoto wengine na jamii kuhusu changamoto kubwa zinazowakumba watoto wa mitaani. Mbinu hii ya mradi iligawanya changamoto hizi katika mchakato wa makundi manne:

1. Sababu zinazopelekea watoto kwenda kuishi mtaani
2. Changamoto wanazokumbana nazo watoto wanapo kuwa mtaani
3. Suluhisho litakalo saidia watoto kutokwenda kuishi mtaani
4. Matokeo ya kiujumla ya kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kijamii.

Washiriki wote 50 walitoa mapendekezo yao kwenye kila kipengele. Wazo la kila mmoja lilijadiliwa sambamba na wachangiaji kujielezea mawazo yao. Baada ya kila wazo kuorodheshwa, kundi likapigia kura masuala muhimu matano kwenye kila kipengele. Mambo haya yakaunda

msingi wa taarifa/mada ya washiriki juu ya suala kuu/ jambo. Wachoraji walitumia mada/ taarifa hiyo kutengeneza picha kubwa tatu zilizoakisi mada pendekezwa. Picha hizi kubwa tatu zilitumika kwa kiasi kikubwa kwenye shughuli za usimamizi na tathmini, lakini pia ziliwekwa nyuma ya jukwaa wakati wa mchezo.

## HITIMISHO

Kwenye miradi ya kisanaa maranyingi kunakosekana usawa kato ya fani (umbo la sanaa) na maudhui (masuala ya yanayopangwa kufanywa). Cre8 imefanikiwa kutengeneza usawa kwenye suala hili kwa kuwahusisha wataalamu kwenye kada tofauti tofauti. Ni muhimu kama wazo au mada ya mradi, ambayo itawasilishwa kwenye onyesho, itaweza kubainisha masuala ya kimaendeleo ya washiriki. Lazima iwasaidie kutatua changamoto zinazowakabili, na wakati huo huo kuwasaidia kutambua na kuonyesha vipaji vyao. Mradiunapaswa kutoa hamasa na kuburudishha watazamaji, lakini pia kuhamasisha na kutoa elimu juu ya mambo ya kimaendeleo kama yalivyobainishwa na washiriki.



## MAMBO YA KUZINGATIA HAPA

- Taarifa kutokana na majadiliano.
- Orodha ya mambo makuu au changamoto kama zilivyoorodheshwa na washirki.
- Orodha ya sababu zote zinazosababisha changamoto zilizoorodheshwa na washiriki.
- Orodha ya masuluhisho juu ya changamoto zilizoorodheshwa na washiriki.



# HATUA YA SITA:
## MAANDALIZI YA UWASILISHAJI (KUFANYA ONYESHO)

Cre8 in 8

*Kutengeneza kwa pamoja*

## UTANGULIZI

**Uwasilishaji ni hatua ya juu kabisa ya mchakato wa "Cre8 in 8". Uwasilishaji unatumia mtindo wa onyesho au wakati mwingine muunganiko wa maonesho, maonesho ya sanaa ya uchoraji (ikijumuisha picha na filamu), mjadala wa wazi na warsha. Ni kwa kupitia uwasilishaji ambapo mchakato na mada vinaaafikiwa na kushirikishwa. Uwasilishwaji ndo kitu kinachotoa fursa ya mradi kujulikana kwenye jamii au watazamaji. Mbali na kukagua usanii wake na thamani yake, wanaweza wakajifunza kutokana na sanaa hiyo. Uchaguzi wa namna ya uwasilishaji na mkakati ni mambo ya muhimu. Njia ya ushirikishaji na kujumuisha fani nyingi kwa pamoja ndiyo inayopendekezwa zaidi. Itasaidia kujumuisha sanaa mbalimbali na vipaji kwa wakati mmoja, itawezesha washiriki na watazamaji kupata jukwaa la pamoja la kushirikishana mawazo kuhusiana na mada inayowasilishwa.**

## YALIYOMO NA MIONGOZO

Kuhakikisha uwasilishaji mzuri, washiriki wanapaswa kuwa na mambo makuu matatu:

1. **Heshima na kujiamini**. Hii inaweza kudhihirika kwa namna washiriki wanavyoshirikiana kwenye mchakato wa kufanya maamuzi. Ni muhimu kuhamasisha washiriki kuwa na mtazamo chanya na kujiamini.

2. **Kuwa na ujuzi wa kisanaa**. Uwasilishaji unapaswa kutoa fursa kwa washiriki kuonyesha vipaji (ujuzi) walivyonavyo. Walimu wa vipaji wanapaswa kutazama namna washiriki wanavyotumia vipaji vyao katika zoezi la uwasilishaji.

3. **Kujenga uelewa**. Kupitia maswali na kutazama kwa kina wanaweza kukusanya taarifa na kuja na jibu/suluhisho lao wenyewe. Hii itasaidia washiriki pamoja na watazamaji kufikiria juu ya hali zao na za jamii zao wakihusianisha na ulimwengu mzima. Kujiamini kwa mtu katika kutoa wazo binafsi ni kielelezo muhimu sana katika hatua hii.



Hatua hii katika shughuli za mradi mara nyingi ni hatua inayo sumbua sana/ inayokera. Umakini ni jambo la muhimu na kuongozi wa sanaa anapaswa kuwa makini na awajibike katika kusimamia na kuongoza mchakato mzima huhakikisha kila mmoja anashiriki kutoa mchango. Mwalimu wa sanaa ana kazi kubwa ya kufanya hapa, hususani katika namna ya kuwasaidia washiriki kuunda sanaa zao kwa pamoja walizoziandaa ili kuunda kwa pamoja mwongozo/ muhtasari wa uwasilishaji. Sambamba na kujijengea uwezo, washiriki wanaweza kubebba majukumu ya walimu na kuongozi wa sanaa na kuyatekeleza kwa naiba yao pale ambapo hawapo..

4. **Kuandaa muongozo wa onyesho**
   Agiza washiriki kutumia ujuzi wao wa kisanaa waliojifunza na changamoto walizozibaini kuja na onyesho fupi. Wanaweza kufanya hivi kwa kundi zima au hata kuwagawanya kwenye makundi madogo madogo ambapo kila kundi litakuwa na kazi yake. Chukua siku 2 au 3 kufanya zoezi hili.

**MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA KUFANYA UWASILISHAJI/ ONYESHO ...**

- Ni muhimu kwamba jambo lolote la kisanaa lililofundishwa liwasilishwe makusudi kabisa , na isitokee limeahirishwa kwa lengo la kusogeza onyesho mbele.
- Ni muhimu kuhakikisha kuwa ujuzi/vipaji vya washiriki vinatambuliwa na wanapata nafasi ya kuvionyesha.
- Ni muhimu kuhahikikisha washiriki wanachukuliwa kwa mtazamo chanya na kuheshimiwa.
- Ni muhimu kuhakikisha kunakuwepo na utendaji wa kila mmoja katika kufanya uwasilishaji. Hii inaweza kufanikishwa kwa kuwapa washiriki majukumu na kazi tofaui tofauti, kwa mfano kwa kumpa majukumu mmoja wao kusimamia suala la nguo za kufanyia sanaa n.k.
- Ni muhimu kwa tamasha/uwasilishaji wa mwisho kuwa wa ushirikishwaji asilimia mia, kwa washiriki kutenda/kuwasilisha kama walimu/wawezeshaji.
- Ni muhimu onyesho lisichukue muda mrefu sana (mfano lisizidi dakika 30 kwa onyesho linalofanyika kwenye jamii au kwenye tamasha) linapaswa kuwa na uwiano katika ucheshi/furaha, nishati/nguvu, uwezeshaji na uhusiano na watazamaji.
- Ni muhimu onyesho liwe na uwezo wa kulenga makundi mbalimbali yta watu: halipaswi kuonekana ni la kiovu au kiuchochezi bali liweze kuwa chanya kulingana na kanuni na taratibu za kijamii na kiutamaduni bila kupingwa kwa namna yoyote ile. Washiriki wananafasi kubwa katika kushauri.
- Ni muhimu kuhakikisha kuwa onyesho linapangiliwa vizuri, lenye ubora wa hali ya juu na liwe la kipeke ili liweze kuvuta hisia za watu wa eneo husika.

**5. Mazoezi ya kutosha**

Kulingana na mahitaji ya onyesho, mkurugenzi wa sanaa huandaa ratiba ya mazoezi. Mazoezi yanaweza kuwa:

1. Matukio ya pamoja ya nayo husisha washiriki wote wa makundi. Mfano pale makundi yanapokuja pamoja kuunganisha vipengele mbalimbali huku wakiongozwa na mkurugezi wa sanaa.
2. Matukio maalumu/binafsi yanayohusiha washiriki walioteuliwa, mfano pale mkurugenzi anapomuomba mwalimu wa vipaji asimamie maendeleo ya fani mbalimbali.

**6. Mavazi, muziki/vifaa vya muziki, mapambo na vifaa vya kufanyia onyesho**

Mkurugenzi wa sanaa, timu ya uzalishaj, timu ya michoro, timu ya vyombo vya mawasiliano na mavazi wakusanyike pamoja kujadili mavazi yatakayotumika, aina ya mapambo ya kutumika na namna onyesho litakavyo fanyika kwa hadhira. Vyombo vya mziki na mapambo vitategemeana na aina ya onyesho ambalo washiriki waliloandaa. Ni muhimu sana kuwahusisha washiriki kwenye kila mjadala utakaofanika.

**7. Pitio la kiufundi la onyesho**

Ni muhimu kuweza kupitia kazi angalau mara 2 au 3, ukijumuisha kuikagua kiufundi, kabla ya kuiwasilisha mbele ya watazamaji. Kila baada ya kufanyia zoezi, kaeni chini pamoja na timu ya mradi na mpeane kila mmoja mrejesho, hususani kwenye maeneo ya marekebisho. Kama haitoshi, mnaweza kufanyia mazoezi baadhi ya vipengele ili kuiweka sawa kabla ya kuipitia tena. Kwenye hatua hii, washiriki wanapaswa kuwa na onyesho lao. Meneja wa jukwaa (inapendekezwa wawe wawili: mvulana na msichana) wanapaswa kuteuliwa miongoni mwa washiriki.



**Kuandaa onyesho la mwisho**

Sehemu ngumu sana kwenye hatua hii ni kuja na mtiririko wa visa na katika onyesho. Cre8 imekuwa ikitumia mbinu tofauti mbili, kama zinavyoelezewa kwenye mifano hii:

**MFANO**

**1. Njia ya kuunda visa**

Kwenye mradi wa "Ngimana Mabiro", Kisumu Kenya washiriki wa makundi walialikwa kusimama kwenye duara. Mmoja wao akaanzisha hadithi/kisa kwa sentensi moja:

> *Mvulana aliyejulikana kwa jina la Okoth alikua anatembea ovyo sokoni…*

Mshiriki mwingine aliyefuatia akaiendeleza hadithi alipoishia wa kwanza, akaongeza sentensi ya pili baada ya ile ya kwanza:

> *Alikua na njaa na amechoka, akaona matunda yanauzwa…*

Hii iliendelea kwa takribani dakika 3, kwa kila mshiriki aliyefuata kuongeza sentensi moja kwenye kisa/hadithi. Kwenye kila jambo washiriki waliongozwa na wazo la mradi lililohusu uhaba wa ajira kwa vijana ambalo walilianzisha kwa pamoja kabla ya zoezi hili. Mkurugenzi wa sanaa baadae akamuagiza mtu mmoja kuielezea story nzima kama ilivyo tengenewa kwa pamoja na kundi..

*Kwenye mbinu hii, Mkurugenzi wa sanaa baadae anawasaidia kundi kuboresha kisa/hadithi kwa kupanga matukio na kufanya kazi kiubunifu kupitia mtiririko wa visa, kurejelea mambo ya kisanii yaliyofanyika kwenye mazoezi kutengeneza kiini cha onyesho/tamasha. Kwa mfano, hadithi/kisa kinaweza kuanza katika hali ambayo hakuna mvua na watu wana njaa. Washiriki wanaweza kucheza ngoma waliyoitunga kuakisi uhalisia, kwa kutumia muziki wenye huzuni uliotungwa na kundi la muziki kuakisi hali halisi … Mchakato huu unaendelea mpaka onyesho lote linakamilika.*

**2. Mbinu ya kufanya onyesho dogo katika kundi**

Mbinu hii ilitumika wakati wa mradi wa "Kati Atyer" huko Gulu, Kaskazini mwa Uganda. Mkurugenzi wa sanaa aliwagawa washiriki 60 katika makundi 5 ya sanaa, waakati huo huo mambo/changamoto zimeshabainishwa. Kila kundi lilipewa kazi kuandaa onyesho fupi kwa kutumia fani za kisanaa moja au zaidi kwa dakika 15 tu kuhakikisha wanabakia kwenye mtiririko wa visa/hadithi na kujaribu kuzuia hali ya kuridhika.

Makundi yaliagizwa kufanya maonyesho waliyoandaa kwa takribani dakika 5 kila kundi. Kwa kutumia migawanyo mitano na kwa msaada wa Mkurugenzi wa sanaa, kundi zima likaunda kisa kimoja chenye mantiki.

*Kwa njia hii ya "kujenga kisa" Mkurugenzi wa sanaa anasaidia kundi kutengeneza onyesho kuu/la mwisho kwa kuunganisha vipengele tofauti tofauti vilivyoundwa na washiriki kwa kutumia usanii wao.*

## HITIMISHO

Maeneo muhimu matatu yakujenga uwezo- **kujiamini, ujuzi binafsi wa kisanaa** na **kujenga uelewa** - yanaunganishwa ili kuunda mada ya mradi – ujumbe mahususi wa kutia hamasa kuhusu changamoto- kwa kufanya onyesho la kibunifu. Kuna njia mbalimbali za kukamilisha hatua za mwisho za onyesho, lakini lazima kuhakikisha mchakato wa majadiliano unazingatiwa na unahusisha wote. Matokeo hayapaswi kutegemewa tu bali yatokane na mchakato wa majadiliano wa pamoja.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA HAPA

- **Onyesho/Tamasha.**
- **Andiko la kisa (kuandaa visa).**
- **Msimamizi/ meneja wa jukwaa.**
- **Orodha ya mavazi, masuala ya muziki na vifaa vya mwanga pamoja mapambo.**
- **Kisa cha kiufundi.**
- **Washiriki wanaopaswa kufanya onyesho.**



# HATUA YA SABA:
## ONYESHO

Cre8 in 8

*Mafanikio yanakaribisha sherehe*

## UTANGULIZI

**Mafanikio ya mradi yatatathminiwa kulingana na ubora/umakini wa onyesho kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa kwenye mpango mradi. Maandalizi ya onyesho yanaweza kuchukua muda sana. Inapendekezwa kuandaa onyesho mapema (mfano, kukodi eneo, kupata kibali, kukodi vifaa vya muziki na mwanga) na si kusubiri mpaka dakika za mwisho.**

### YALIYOMO NA MIONGOZO

Idadi ya maonyesho yatakayofanyika itategemeana na mpango mradi na muundo. Jambo la msingi sana si idadi ya maonyesho bali jambo la msingi ni aina ya onyesho, kama ilivyopendekezwa na watazamaji na hali halisi ambapo onyesho litafanyika.

Kwenye kila mradi, Cre8 waliandaa aina zifuatazo za maonyesho:

**Onyesho la rika**. Hii aina ya onyesho inalenga watazamaji wenye rika sawa na washiriki. Ni matamasha muhimu na inapendekezwa kufanya onyesho lako la kwanza liwe onyesho la rika na kulifanya kwenye oneo la mazoezi. Unaweza pia kufanya pitio la onyesho lako la mwisho kama onyesho la rika.


**Onyesho la kwenye jamii.** Aina hii ya onyesho hufanyika ndani ya jamii, hususani maeneo ya sokoni, kando ya barabara ya kijiji yenye watu wengi au kwenye uwanja wa kijiji.

**Onyesho la wahisani/wadau.** Hii aina ya onyesho inajulikana pia kama onyesho kwa viongozi wanaotoa mapendekezo ambalo linajumuisha viongozi wa mtaa, watendaji wa shughuli za kimaendeleo, wataalamu wa eneo husika na wengine waliopo katika kufanya maamuzi katika ngazi tofauti za jamii. Onyesho hili linaweza kufanywa katika ukumbi wa mtaani au likafanywa na mmoja wa wahisani kwenye jamii.

**Onyesho la umma.** Haya ni maonyesho makubwa yanayokusanya watazamaji mbalimbali. Mara kwa mara yanafanywa maeneo ya mjini, kwenye uwanja au maeneo ya maegesho, ili kuwezesha watu wengi kuweza kuona.

Moja kwa moja baada ya onyesho, utafiti juu ya tathmini kutoka kwa watazamaji lazima ufanyike. Ni muhimu kukusanya maoni/matazamo kutoka kwa watazamaji si tu kwa namna walivyo vutiwa






na onyesho kwa ujumla, bali pia kwa jambo/suala ambalo limeonyeshwa. Maswali muhimu ya tathmini yanaweza kuwa:

- Umependa/ kufurahia onyesho, Ndio/ Hapana? Kama ndio kipi umekipenda zaidi?
- Unamtazamo gani kwa washiriki juu ya washiriki kulingana na vipaji vyao? Wana vipaji? Kama ndio vipaji gani?
- Umejifunza chochote kutoka kwenye onyesho? Ndio. Taja vitu vitatu ulivyojifunza.
- Una mawazo yoyote juu ya kuboresha mradi huu?

Hakikisha washiriki wanakusanyika pamoja kila baada ya onyesho kutathmini na kutoa maoni/mrejesho juu ya walichokiona kwenye onyesho. Hii itasaidia kuangalia kama onyesho limefanikisha

kufikia malengo yake kama ilivyo kwenye mpango mkakati.

## MFANO

Wakati wa mradi wa AMKA, kundi lilisafiri Tanzania na Kenya kufanya matamasha miji saba tofauti. Kila onyesho lilikuwa tofauti kwa sababu kuu mbili. Jambo la kwanza, watazamaji walikuwa tofauti kabisa. Wakati mwingine tulitengeneza onyesho kwa watazamaji wa rika sawa na washiriki, wakati mwingine tulifanya onyesho kwa wadau/wahisani/ au kwa jamii husika, na wakati mwingine tulifanya onyesho la umma. Kundi liliwasiliana/husiana tofauti na kila aina ya watazamaji, kwa hiyo kila tamasha lilikua na namna yake na utofauti wake. Sababu ya pili iliyofanya kila tamasha kuwa tofauti ni kwa kuwa wasanii waliwauliza watazamaji maswali kila baada ya onyesho. Matokeo ya kila utafiti yalichochea/ sukuma onyesho lililofuata. Pale ambapo washiriki walihisi watazamaji walikosa ujumbe uliokusudiwa waliweza kujisahihisha kwa kurekebisha baadhi ya vitu/vipengele kufanya ujumbe uweze kueleweka.

## HITIMISHO

Licha ya kuwa ni nyenzo ya uwezeshaji, onyesho/ mradi pia ni chombo cha utetezi. Linalenga kushawishi umma na kuhamasisha watu kuchukua hatua kuboresha maisha ya jamii.

Hivyo kwa wanajamii, kupata fursa ya kutazama onyesho na kukutana na waandaji wa onyesho hilo (washiriki) inamaanisha kwamba matokeo ni ya haraka na hivyo inawapa chachu ya kuchukua hatua. Mradi unalenga kwa watu wote. Hii ndo sababu kuu tamasha lilifanyika kwenye maeneo ambayo watu walijisikia huru na kujieleza kwa uwazi.



## VITU VYA MSINGI HAPA

- **Orodha (ratiba) ya maonyesho.**
- **Mpangilio wa vifaa.**
- **Orodha ya vitu vinavyohitajika, (au vinavyopangwa kufanywa).**
- **Vibali rasmi.**
- **Fomu za tathmini za watazamaji.**
- **Picha na video za maonyesho.**
- **Muhtasari wa mrejesho kutoka kwa washiriki.**




# HATUA YA NANE:
## UFUATILIAJI NA MPANGO ENDELEVU

Cre8 in 8

*"safari ndefu inaanza na hatua moja; hivyohivyo safari ndefu inaishia na hatua moja... kumbukumbu inaishi milele."*

## UTANGULIZI

**Ni muhimu kuwa na mpango wa ufuatiliaji, kuhakikisha matokeo ya muda mrefu. Waanzilishi wengi wa mradi huwa wanaishia kutokua na muelekeo mzuri, kama si kurudia rudia mafanikio waliyopata kwa sababu ya kukosa mpango endelevu. Kwenye hili, uendelevu haumaanishi kwamba utaendelea kuhusisha washiriki kwenye mambo yao kila siku baada ya mradi, bali mafanikio ya awali na matokeo yaliyoonekana kwenye mradi ndivyo vinavyopaswa kuwa endelevu.**

### YALIYOMO NA MIONGOZO

Kwenye mpango endelevu ni muhumu kwamba:

- Ujuzi utakaopata na uwezo wa kufundisha ujuzi huo utabaki ndani ya jamii kupitia mafunzo yya walimu (TOT)
- Mradi unaambatanishwa na wadau wa jamii ambao wana uwezo kwa kutumia njia/mbinu hii kwenye mipango yao ya kila mara.
- Mpango endelevu au mkakati utaanzishwa unaojumuisha matarajio na hali za washiriki katika kiini cha utekelezaji wake.
- Mpango huu endelevu ni lazima uwe wa kweli/ unaotekelezeka na uwe ndani ya uwezo wa washiriki, wadau wa kwenye jamii na jamii kwa ujumla.

Mpango endelevu mzuri ni sehemu ya mpango mradi, na mwanzilishi anapaswa kuhakikisha wadau wote wanahabarishwa.

### MFANO

Moshi, Tanzania Cre8 walifanya kazi na menejimenti ya Mkombozi kuhakikisha kunakuwa na ufuatiliaji na kuwa matokeo yanapaswa kuwa endelevu. Kufanya kazi kulingana na mikakati iliyokubaliwa, Mkombozi ilirasimisha mradi wa Cre8 kwenye programu zake, ambapo washiriki waliruhusiwa kukutana mara kwa mara kwenye taasisi hiyo ili kuendeleza ujuzi/vipaji vyao. Mbali na mfanyakazi wa Mkombozi aliyeteuliwa kusimamia mradi huo, walimu/wawezeshaji wa mtaani kama mwalimu wa sarakasi walialikwa mara kwa mara kuongoza washiriki. Mfanyakazi wa Mkombozi aliandika taarifa kila baada ya kipindi fulani juu ya maendeleo ya washiriki na kuwashirikisha Cre8. Baada ya mwaka mmoja, cr8 waliandaa kipindi cha ufuatiliaji wa washiriki kwa ushirikiano na Mkombozi si chini ya asilimia 60% ya washiriki wa awali walishiriki katika kipindi hicho.

Kwa mbinu ya majadiliano kwenye kundi, washiriki walieleza maendeleo waliyopata wakati uliopita tangu kuisha kwa mradi. Waliweza pia kuonyesha baadhi ya kazi zao, ambazo zilionyesha ushahidi ni kwa kivipi ujuzi wao wa kisanii uliendelea lakini pia namna gani uelewa wao wa maendeleo ya mambo umeimarika. Kwa mfano vijana wadogo waliokuwa wanafanya shughuli za uchoraji kipindi cha Cre8 waliweza kuanzisha duka la uchoraji, ambapo wali chora picha na bidhaa nyingine kwa ajili ya kuuza. Walianzisha pia kituo cha mafunzo ya uchoraji na usimamizi kwa vijana wa jamii ile.

### HITIMISHO

Kufikiria juu ya matokeo endelevu ya mradi ni kitu ambacho kinapaswa kutiliwa mkazo kwenye kila hatua ya mradi. Kila maamuzi yanayofanyika yanapaswa kufanywa katika mtazamo wa kuhakikisha matokeo ya muda mrefu/yasiyo na ukomo. Majukumu ya utekelezaji wa mpango endelevu yapo kwa wanufaikaji, ukijumuisha shirika lililosimamia zoezi pamoja na washiriki.

## MAMBO YA KUZINGATIA HAPA

- **Uzingatiaji mzuri wa mpango mkakati.**
- **Makubaliano endelevu na wadau wa kwenye jamii.**
- **Mpango wa usimamizi na tathmini.**

# SHUKRANI

Cre8 Afrika Mashariki inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa wote waliotuwezesha kufanikisha miradi yetu kwa miaka kumi iliyopita: Wote waliotusaidia kukusanya fedha au kuandika maombi au kujitolea kipindi cha kampeni zetu za kukusanya fedha vilevile shukrani kwa wale ambao wamesaidia kiutaalamu kwenye shirika letu, kutengeneza tovuti, kuandika majarida na kubuni miradi yetu. Pia tunashukuru watu wengi walioshiriki katika mradi wetu wa Afrika Mashariki, kwa mfano walimu wa sanaa, wapishi au wasaidizi. Pia tunashukuru wadau wetu na mashirika kutoka Kenya, Uganda na Tanzania. Tunashukuru mamia ya vijana wadogo walioshiriki katika mradi wetu lakini pia ndugu zao waliotuamini kufanya kazi na watoto wao. Mwisho, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa mashirika na msaada kutoka kwa watu binafsi ambao kutokana na msaada wao wa kifedha na kimawazo, wametuwezesha kufanya kazi na watu wengi kwa mradi ambao kiukweli hautosahaulika.

Cre8 Afrika Mashariki tunapenda kukushukuru kwa kusoma mwongozo huu na tunakutakia kila la kheri kwenye kazi zako za mbeleni.

Nairobi / Amsterdam, Januari mwaka 2016


cre8
east africa
education through culture & art